# Wananchi waonywa utupaji ovyo wa taka za plastiki

NA MWANAJUMA MMANGA

**WANANCHI Zanzibar wametakiwa kuacha tabia ya kutupa taka ovyo za palastiki na badala yake kuendelea kuhifadhi na kutunza mazingira ili kuepusha atahari zinazoweza kujitokeza.**

Mkuu wa kitengo cha divisheni elimu ya Mazingira kutoka Idara ya Mazingira, Zuwena Juma, aliyasema hayo wakati akizungumza na mwandishi wa gazeti hili ofisini kwake Maruhubi, wilaya ya Magharibi 'A' Unguja.

Alisema bado jamii haijawa na taaluma ya kutosha juu ya kutenga aina ya taka ngumu, nyepesi na za wastani jambo ambalo hupelekea kuzagaa taka za plastiki na ngumu kuelekea pwani na kuathiri chakula cha samaki matumbawe.

Aidha alisema nchi nyingi duniani huwa wanaweka mazingira ya kuhifadhi aina ya taka, hivyo si vyema jamii ikajifunza namna ya kupambanma na matumizi ya chupa za plastiki ili kuepusha na mabadiliko ya tabia nchi.

Alifahamisha kuwa mabdailiko ya tabia nchi husababishwa na ukataji ovyo wa miti, kwa kisingizio cha upatikanaji wa kuni na mkaa pamoja na uchimbaji wa mchanga hali inayochangia kupanda kina cha maji.

Aliongeza kusema kuwa kupanda kwa kima hicho cha maji ambayo inapelekea kusababisha kuwepo kwa mabadiliko ya tabia nchi.

"Hivi sasa Zanzibar inapambana na uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na taka za palastiki ambao imekuwa hatari katika fukwe za bahari", alisema.

Aliongeza kuwa ni vyema kwa jamii na wananchi kwa ujumla kuwa mabalozi wa kuhifadhi na kutunza mazingira na badala yake kutafuta chupa mbadala kwa ajili ya matumizi ya binaadamu.

Alisema mara hii wameamua kufanya maonesho ya biashara za taka za plastiki kwa lengo la kupambana juu ya athari ya taka za plastiki hasa inaathiri kwa kiasi kikubwa katika maeneo hasa ya baharini.

"Tumefanya kongamano kwa kushirikiana na taasisi zinazopambana na taka za plastiki na NGOs katika kuhakikisha Zanzibar tunaondoa matumizi ya taka za plasti pamoja na matumizi ya mifuko ya plastiki", aliongeza.

Pamoja na hayo, aliwahimiza wadau wa mazingira, NGO's, taasisi za serikali na binafsi pamoja na wafanyabiashara wa bidhaa za palastiki kushajiika kuungana pamoja katika maonesho hayo ili kufanikisha maonesho yanayotarajiwa kufanyika Juni 13, mwaka huu.



*WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Shariff Ali Shariff, akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ajira za Watoto inayoadhimishwa Juni 12 ya kila mwaka hafla iliyofanyika katika ofisi za wizara hiyo, Mwanakwerekwe Zanzibar. (PICHA NA FAUZIA MUSSA).*

# Wananchi wataka elimu zaidi masuala ya sheria

NA ASYA HASSAN

**TAASISI, wadau wa sheria na wanaharakati wametakiwa kuongeza juhudi katika kuielimisha jamii kuhusu haki za wanawake na watoto, hususan kwenye masuala ya mirathi na udhalilishaji.**

Wito huo umetolewa na wafanyabiashara wa soko la Jumbi baada ya kupokea mafunzo ya elimu ya kisheria kutoka Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA) kwa ushirikiano na Taasisi ya Kuwawezesha Wanawake Kielimu na Kiuchumi Zanzibar (FAWE) na kueleza hatua hiyo itaondoa uonevu unaoendelea kuwakumba wengi katika familia na jamii.

Walisema bado wanawake hasa wajane na waliotelekezwa na waume zao wanakumbwa na ukandamizaji mkubwa wa haki zao ambapo baadhi ya ndugu wa marehemu hujitokeza kudai mali.

Walisema hali hiyo huwaacha wanawake na watoto katika mazingira ya fadhaa na wakati mwengine kutengwa kijamii.

"Tunapongeza taasisi hizi kwa kutufikia, elimu hii itatusaidia wanawake wengi kudai haki zao kisheria badala ya kufumbia macho dhuluma tunazokumbana nazo", alisema Khamis Ibrahim, mfanyabiashara soko la Jumbi.

Alisema elimu hiyo imewafumbua macho na watakuwa mstari wa mbele kuwasaidia wanawake ambao wanakutana na changamoto hizo na kuwaacha watoto wakiteseka bila msaada wowote.

Mfanyabiashara mwengine Aidan Ngoromelo, aliomba elimu hiyo kuwa endelevu na kuwafikia wananchi wa chini kwani wengi wao ndio waathirika wakubwa wa matukio hayo.

Kwa upande wake Hakimu wa Mahakama ya Watoto mkoa wa Kusini Unguja, Naila Abdulbasit, alisema serikali pamoja na Mahakama zinaendelea kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wanawake, watoto na jamii kwa ujumla.

Naye Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo mkoa wa Kaskazini Unguja, Saumu Mohamed, alisema jamii ina wajibu wa kutoyavumilia matendo ya ukiukwaji wa haki kama vile udhalilishaji, migogoro ya mirathi, wasia na masuala ya ardhi.

Mafunzo haya yameelezwa kuwa sehemu ya mkakati wa kuimarisha utawala wa sheria na kupunguza dhuluma zinazowakumba wananchi, hasa wanawake, kwa kuwapa maarifa ya kisheria yatakayowasaidia kudai haki zao kwa ujasiri na uelewa yanafadhiliwa na Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa (UN Women).

# Wafanyabiashara mazao ya kilimo watakiwa kuzingatia sheria

NA SALAMA MOHAMMED, WKUMM

**MKUU wa Karantini na Ukaguzi wa mazao kutoka Idara ya kilimo na uhakika wa chakula Zanzibar, Khamis Maulid Mohamed, amewashauri wafanyabiashara wanaoingiza na kusafirisha biashara za mazao ya kilimo ndani na nje ya Zanzibar kupitisha biashara zao kupitia maeneo yaliyoruhusiwa kisheria.**

Khamisi alieleza hayo hivi karibuni aliposhiriki kipindi cha Mazungumzo ya Asubuhi kinachoendeshwa na Kilimo TV alitaja maeneo hayo kuwa ni pamoja na bandarini na viwanja vya ndege ambayo ni rahisi kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi kabla kufika sokoni pamoja na kumfikia mlaji.

Alisema kuzingatiwa kwa afya ya mimea ni jukumu la kitengo hicho na jamii kwa ujumla kila mfanyabiashara aa wajibu wa kupitisha katika sehemu rasmi na kuepukana na mashambulizi ya wadudu na maradhi kwa mazao ya wakulima ndani ya nchi.

"Lengo la uwepo wa watu wetu katika bandari ni kuchunguza mazao yanayoingia na kutoka nchini kubaini kama haijavamiwa na wadudu au visababishi vya maradhi na kuepuka usambazaji wa visumbufu katika mazao", alieleza Khamis.

Aliongeza kuwa hatua hiyo inalenga kuwalinda wakulima wanaolima mazao mbali mbali wapate faida na kuongeza uzalishaji wa mazao bila uwepo wa wadudu ili kuhakikisha bidhaa inapoingia nchini inafanyiwa uchunguzi na kua salama.

Aidha alifahamisha kuwa suala la uchunguzi halipo Tanzania peke yake bali lipo duniani kote ambapo kuna vitengo vinavyofanya uchunguzi wa bidhaa zinazoingia nchini ikiwa ni sehemu ya makubaliano ya kimataifa.

"Mazao ya kilimo pindi yanapoingiza bidhaa za mazao wanaziangalia ili kuepuka matatizo na kwa upande wa nchi ya Tanzania Zanzibar na wao wanapopeleka bidhaa zao nje ya nchi na wao hawapokei matatizo yaliyomo katika mazao yetu", alieleza Khamis.

Aliongeza kuwa; "Hatuwezi kuruhusu Kuingia bidhaa zisizo na kiwango nchini kwani kisumbufu kidogo tu kikiwa katika mmea au matunda kinaweza kuenea nchi nzima na hivyo hupelekea athari mbaya kwa wananchi na taifa kwa ujumla".

Hivyo aliwasisitiza wakulima wajitahidi kuzalisha mazao yenye ubora ili yaweze kua Salama kwao bila kupata matatizo katika usafirishaji pamoja na kukata vibali ili kuepusha usumbufu wanapoingiza mazao yao katika maeneo yaliyopo kisheria

Aliongeza kuwa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kupitia kitengo cha ukaguzi wa mazao itaendelea kutekeleza sheria namba 9 ya mwaka 1997 inayozungumzia afya ya mimea kwa ajili ya kuangalia usalama wa mazao.

Alifafanua kuwa sheria hiyo pia inazungumzia uwezo wa wakaguzi wa mazao yanayoingia nchini sambamba na uzingatiaji wa sheria za kimataifa ikiwemo na miongozo ya kikanda na kwamba kila sheria inampa mkaguzi muongozo wa kila hatua za ukaguzi juu ya bidhaa zinazopitishwa katika maeneo yaliyowekwa kisheria.